

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



Septemba 21, 2022

**MKUU WA WILAYA YA LUDEWA AMEONGOZA KIKAO CHA PEMBEJEO**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere akiwakilishwa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa Bw. Linus Malamba leo Septemba 21, 2022 ameongoza kikao cha Pembejeo kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa.

Kikao hicho kimehudhuliwa na viongozi mbalimbali wa Kamati ya Pembejeo akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ludewa Ndg. Sunday Deogratias ni Katibu wa Kamati ya Pembejeo lakini pia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Ludewa imeshiriki kikao hicho.

Pamoja na mambo mengine Afisa Kilimo (W) Ludewa Bi. Clementina Kabaka amewasilisha taarifa ya mwenendo wa usajili wa mbolea ya Ruzuku kwa Wilaya ya Ludewa na kuweka mkakati wa kufanikisha upatikanaji wa mbolea ya Ruzuku kwa wakulima kwa wakati.

Wakati akihitimisha kikao hicho Katibu Tawala wa Wilaya ya Ludewa amesema kuwa, ***“Nitumie nafasi hii kuwatahadharisha watu wote watakaojitokeza ama mtu yeyote anayepanga kuhujumu zoezi hili la Mbolea ya Ruzuku kuacha mara moja, kwani Serikali iko macho muda wote kuona zoezi hili linatekelezeka kama lilivyo kusudiwa kwa kuwafikishia wananchi wote kwa maeneo yote kwa kufuata taratibu na miongozo iliyotolewa, hatutaona haya kwa mtu yeyote kumchukulia hatua za kisheria endapo akabainika kuhujumu zoezi hili”***. ameyasema Bw. Linus Malamba.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Chrispin B. Kalinga'.

**Chrispin B. Kalinga**  
**Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini**  
**Halmashauri (W) Ludewa.**